

## Lugha na Utandawazi: Nafasi ya Kiswahili katika Kukuza na Kuendeleza Demokrasia Nchini Kenya

Kimathi Mwembu<sup>1</sup> na Mwenda Mukuthuria<sup>2</sup>

<sup>1</sup>Chuo Kikuu cha Chuka, Kenya

<sup>2</sup>Chuo Kikuu cha Maasai Mara, Kenya

### Ikisiri

Lugha huwa na nafasi kubwa katika maisha ya jamii huku mawasiliano yakiwa mojawapo wa majukumu yake. Awali, jamii mbalimbali zilikuwa zikijichukulia kama kwamba zimejitenga na jamii nyingine zikiwa na jinsi ya kufanya shughuli zao kivyao. Hii leo, utandawazi umekita na kila jambo linatazamwa kwa muktadha wa dunia kuwa kijiji. Demokrasia ni falsafa ya kisiasa inayoenea kote duniani kwa haraka. Kwa misingi hii, falsafa inatakiwa kuchanganuliwa kwa mujibu wa taaluma zingine za utamaduni kama vile lugha. Kwa hivyo, makala hii inanua kubainisha nafasi ya lugha katika kukuza demokrasia na uongozi mwema. Inapendekeza matumizi ya Kiswahili na lugha za kiasili kama nyenzo za kukuza na kueneza demokrasia katika muktadha wa bara la Afrika. Pia, inaangazia jinsi taasisi za kijamii kama katiba, mahakama, tume za uchaguzi, vyombo vya habari na makundi ya kutetea haki za kijamii yanavyotumia Kiswahili kutetea na kuendeleza demokrasia. Inatazamiwa kwamba makala hii itachangia upanuzi wa maarifa katika taaluma ya isimu-jamii, hasa nyanja za uongozi na utawala na majukumu ya lugha. Hatimaye makala hii inapendekeza kwamba lugha ya Kiswahili itumike kufundisha somo la mawasiliano katika ngazi ya chuo kikuu ili kutilia nguvu matumizi yake na wataalamu wanaohitimu katika nyanja mbalimbali.

Maneno Muhimu: *Utandawazi, Lugha, Demokrasia, Maendeleo*

### Utangulizi

Maendeleo makubwa katika uwanja wa teknolojia ya habari na mawasiliano yamewezesha wanadamu kuwasiliana kwa urahisi pasi na kutatizwa na kizingiti cha masafa yaliyoko baina yao. Mawasiliano rahisi baina ya watu kutoka sehemu za mbali na maeneo tofauti yamesababisha kuzuka mitazamo ya kijumla kuhusu masuala yanayomhusu takribani kila mwanadamu. Katika harakati ya kutaka kufanya mambo kwa jinsi moja, na vilevile kusawazisha hali fulani, suala la ujirani wa kiulimwengu limezuka. Watu wamejaribu kupanga mambo upya na vilevile kwa njia sawa kama kijiji kimoja. Ni katika hali hii ambapo suala la utandawazi limezuka. Utandawazi

umefanikiwa kutokana na mihimili mitatu inayozunguka maisha ya mwanadamu. Yaani, mhimili wa kitamaduni, kisiasa na kiuchumi. Kati ya mihimili hii mitatu inayoshikilia utandawazi, ule wa kisiasa una nguvu nyingi na ushawishi mkubwa. Siasa huchangia pakubwa katika kutoa mwelekeo wa maendeleo ya kijamii na vilevile ya kiuchumi katika nchi. Maendeleo ya kisiasa katika mtazamo wa utandawazi yanaweza kuchukuliwa kuwa hali ya kuzingatia maongozi ya kidemokrasia na utawala wa sheria. Makoti (2008) anasema kwamba maendeleo huletwa na wasomi na wataarazi ambao wana elimu ya kijamii, kisayansi na kiteknolojia. Wataalamu hawa lazima wawafundishe wanajamii wengine kwa kutumia lugha inayoeleweka. Hii ni kwa sababu bila matumizi ya lugha inayoeleweka, mawasiliano hayapo. Hapa Afrika Mashariki, Kati na Kusini, lugha inayofaa kuleta maendeleo ya kisiasa ni Kiswahili. Chimera (1998) anashadidia kauli hii anaposema kuwa Kiswahili ni lugha sambazi na imesheheni msamiati mpana. Akimrejelea Kiango, Msanjila (2005) anasema kwamba Kiswahili kimevuka mipaka ya nchi zao asilia yaani Tanzania na Kenya na kuenea karibu kwenye nchi zote Afrika Mashariki na Kati japo kwa viwango tofauti. Hakuna lugha nyingine ya Kiafrika katika nchi hizi za Afrika Mashariki yenye sifa kama hiyo. Kauli ya msomi huyu imesadifu kuwa ukweli kwa kuwa hii leo, Kiswahili kina hadhi ya lugha rasmi na lugha ya taifa katika nchi ya Kenya na Tanzania; hadhi ya lugha rasmi nchini Uganda na Rwanda; na kisera, ni lugha ya Jumuiya ya Afrika Mashariki. Kabla ya kujitoma katika mjadala wa ukuzaji wa demokrasia na lugha ya Kiswahili, tutaangazia dhana za utandawazi, demokrasia na lugha.

### Utandawazi

Dhana ya utandawazi ni nyeti ya kujadiliwa kwa sababu huwa na mitazamo tofauti. Kulingana na Kamusi ya Kiingereza ya Oxford (1989) utandawazi ni mtazamo unaoyaona maeneo mbalimbali ya ulimwengu kama eneo moja ambalo utaratibu wa kuendesha shughuli za kila siku huwa karibu sawa. Katika mwelekeo huu, shughuli za kila siku zinazofanywa kwa njia sawa huhusu mambo mengi. Miongoni mwa mambo hayo ni kutumia lugha moja au mbili ambazo ni sambazi; na kuzingatia uongozi wa kidemokrasia. Vilevile, utandawazi unahusu matumizi ya sarafu moja katika biashara ya kimataifa; pamoja na kutungwa na kuzingatiwa kwa sheria za kimataifa. Aidha, kuibuka kwa utamaduni wa aina moja; na wakati huo huo watu kushiriki katika tamasha za kimataifa kama vile michezo ya Olimpiki. Na hatimaye kuwepo kwa elimu na maarifa ya kiteknolojia yaliyofanana katika kila pembe ya dunia. Shirika la Fedha la Kimataifa linasema kuwa utandawazi ni tukio la kuunganishwa kwa karibu kwa masoko ya bidhaa na huduma na vilevile mtaji (IMF, 1997:112). Bila shaka huu ni mtazamo wa kiuchumi. Kihore, akirejelewa na Msanjila (2005), anasema kwamba, jambo lililo dhahiri kuhusu utandawazi ni kwamba, hii ni dhana yenye asili yake katika nchi za magharibi.

Mwanazuoni huyu anaendelea kusema kwamba mataifa haya ni yaliyokaliwa na Wazungu huko Marekani Kaskazini na Ulaya. Nchi hizi ziliazimia kuhifadhi uwezo wao wa kiuchumi kwa kila namna. Mojawapo ya hatua nchi za kimagharibi zilizochukua ili kudumisha ubabe wao wa kiuchumini ni kuanzisha mfumo wa ukoloni-

mkongwe; na hatimaye ukafuatiwa na ukoloni-mamboleo. Katika hali hii, watu wanaopinga utandawazi wanauchukulia kuwa ndicho kiwakilishi kikubwa cha mfumo wa ukoloni-mamboleo. Mtazamo huu umeshadidiwa na kauli kwamba utandawazi umejengwa katika misingi mipya iliyoibua masharti mapya ya uendeshaji wa mambo yaliyoimarishwa kisheria. Sheria zinazoongoza utandawazi hivi leo zinaundwa na mataifa yenye ushawishi mkubwa, hususan yale ya Kimagharibi (Msanjila, keshatajwa). Kwa kuzingatia mtazamo wa utamaduni, wanazuoni wanasema kwamba utandawazi kuhusiana na utamaduni hutokea wakati ambapo kuna msambao wa mawazo, mielekeo na maadili kutoka nchi moja hadi nyingine ([www.wikipedia.org](http://www.wikipedia.org)). Ni vyema kutaja kwamba msambao wa tamaduni haujaanza leo, umekuwepo tangu zamani ila tu ulitokea kwa mwendo wa polepole kwa sababu wakati huo teknolojia ya mawasiliano haikuwa imeboreka. Hali ya kusambaa na kubadilishana maarifa husababisha watu kuungana kwa urahisi na pia kutagusana kwa watu wenye tamaduni anuai na maisha tofauti.

Katika mtazamo wa kisiasa, utandawazi ni mwongezeko wa idadi ya tawala na mamlaka zinazojumuika pamoja ili kuathiri mwelekeo wa jinsi dunia inavyotawaliwa. Wakati nchi kadhaa zinaungana kushinikiza nchi nyingine kufuata maongozi yanayopendelewa na wengi ulimwenguni, basi tunaweza kusema huo ni utandawazi wa kisiasa. Jambo la kuajabia kuhusu utandawazi ni kuwa miundo, mifumo na hali ambazo huathiri wanadamu huwakumba na kuingia katika utaratibu wa kila siku pasi na wao kuipinga hata ikiwa wangepata nafasi ya kufanya hivyo. Kwa njia nyingine, utandawazi ni wimbi ambalo halizuiliki kamwe. Ni katika hali hii ambapo lugha ya Kiswahili inapaswa kuendelezwa na kukuzwa huku ikishirikishwa katika nyanja zote ambazo zinaathiriwa na utandawazi, badala ya kuachia jukumu hilo lugha za kigeni. Kwa jumla, utandawazi hurejelea usawazishaji wa kuendesha mambo, miundo ya kijamii na hata hali mbalimbali.

### **Demokrasia**

Utandawazi unasheheni mambo mengi. Baadhi ya mambo haya ni demokrasia. Dhana ya demokrasia inazua msisimuko mkubwa. Hii ni kwa sababu watu mbalimbali huwa na mitazamo tofauti kuhusu namna demokrasia halisi inapaswa kuwa. Demokrasia ni neno linalotokana na neno la kigiriki “demokratia” ambalo likichanganuliwa linaleta neno “demos” maana yake watu, na neno “kratos” maana yake utawala au mamlaka. Mintarafu ya hayo, kumekuwa na mitazamo tofauti kuhusu matumizi ya neno ‘demokrasia’. Yuen (1988) akijadili maoni ya watu mbalimbali kuhusu demokrasia anasema kuwa kuna wale ambao wanadai kuwa demokrasia inatumika kwa maana ya serikali ya mitaa ambayo inaendeshwa na watu ambao wanaishi chini ya serikali kuu. Mfano ni huko Uingereza ambako masuala ya miji yanaendeshwa moja kwa moja na wakaaji wa miji hiyo. Vilevile, Yuen (keshatajwa) anasema, wengine wamedai kwamba demokrasia ni jamii yenye kutawaliwa kupitia kwa wawakilishi ambao wanajali masilahi yao. Pia, wengine wamesema demokrasia ni wakati ambapo uwezo wa kisiasa wa watu wa kawaida unatambuliwa. Katika jamii kama hiyo, huduma kwa wanajamii huwa ni sawa. Kwa vyovyote vile, demokrasia inahusu wanajamii kuwa na

uhuru wa kutenda, kusema, kufikiria na kutekeleza jambo lolote ambalo linanufaisha mtu binafsi ama jamii nzima. Aidha, kuna usawa katika ugavi wa chumo la taifa na pia utoaji wa huduma kiusawa katika jamii.

Katika utawala wa kidemokrasia, sera za uongozi huwa muhimu. Sera ni mwongozo ambao huratibiwa na wataalamu ili kufuatwa na viongozi na watawaliwa. Iwapo wataalamu pamoja na wanasiasa watumia lugha ngeni isiyoeleweka na raia wa kawaida katika kuandika sera zao, basi mfumo mzima wa demokrasia utakuwa umeingia dosari. Hivi ni kusema kwamba, kutunga sera kwa kutumia lugha inayoeleweka ni hatua muhimu inayoweza kuchangia kustawi na kuimarika kwa demokrasia. Katika hali hii, ni vizuri kutambua nguvu zinazopatikana katika lugha. Thiong'o (1986) anasema kwamba lugha ni msingi wa uhusiano miongoni mwa watu katika mchakato wa shughuli zozote zile. Kwa hivyo, lugha ni kiungo muhimu katika maendeleo ya utawala wa kidemokrasia.

### **Dhima ya Lugha katika Siasa**

Tunapojadili dhima ya lugha katika kukuza demokrasia inafaa tujibu maswali haya: Lugha ni nini? Siasa ni nini? Kuna vijelezi tofauti kuhusu lugha. Kamusi ya Workbook (1988:178) inasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti ambazo wanadamu hutoa kupitia kwa ama maandishi au matamshi. Lugha ni kama tabia zingine za mwanadamu ambazo hujifunza kutoka utotoni au ukubwani ambazo ni vigumu kubadilishwa hapo baadaye. Naye Trudgil akinukuliwa na Mgullu (1999) anasema kuwa lugha ni mfumo wa sauti za nasibu zinazotumiwa katika mawasiliano miongoni mwa watu wa jamii fulani yenye utamaduni wake. Labov katika Njogu (2008) anaifafanua lugha kama umbo la tabia za kijamii. Chomsky (1977) anabainisha lugha kama elementi ya kiakili ambayo mtu huipata kwa kujifundisha; na elementi hii hutumiwa na mzungumzaji pamoja na msikilizaji. Mbali na kuiona lugha kama elementi ya kiakili, Chomsky pia anazungumzia muundo wa nje wa lugha; kwa maana ya mkusanyiko wa sentensi zinazoeleweka bila kurejelea sifa za kimutadha. Kamusi ya TUKI (1990) inasema kwamba lugha ni mfumo wa sauti zinazotumiwa na watu wa jamii fulani wenye utamaduni unaofanana ili kuwasiliana. Kijelezi hiki ni mwafaka kwa sababu kinataja jamii na utamaduni unaofanana.

Suala la jamii na utamaduni ni mambo muhimu ya kutilia maanani unapojadili utandawazi. Lugha ni njia ya kueleza maoni na hisia za wanadamu kwa kutumia sauti, maandishi au ishara fulani. Lugha ndicho chombo ambacho kinajenga msingi wa kuwepo kwa upekee wa mwanadamu na pia kushirikisha utamaduni wake. Umadhubuti na fahari ya mwanadamu yeyote yule hupatikana katika lugha yake. Ikiwa lugha ya jamii fulani itauliwa au miundo yake kubadilishwa, basi utamaduni wa jamii hiyo utakuwa umeyumbishwa. Tukio kama hili linaweza kutingisha nguzo za jamii husika kama vile siasa. Hivi ni kusema kwamba nguvu za lugha katika jamii yoyote ile haziwezi kulinganishwa na nguvu zingine zozote. Lugha inaweza kujenga au kubomoa chochote ambacho kinahitajika katika jamii fulani. Uwezo huu wa lugha wa kujenga na kubomoa haupatikani katika chombo au taasisi nyingine ya kijamii. Lugha inaweza kuleta umoja au utengano, kuhimiza au kukatiza ari na pia kueleza uvumbuzi. Lugha

inaweza kutumiwa kufafanua sera za utawala wa kidemokrasia au kuendeleza sera dhalimu za kifashisti. Aidha, inaweza kuupa utamaduni uthabiti au kuudhoofisha. Lugha ni chombo cha kupitisha utamaduni kutoka kizazi kimoja hadi kiingine na vilevile kutumika kupata au kupitisha maarifa (Njogu, 2008).

Jibu la swali “siasa ni nini?” linajikita katika tathmini nzima ya mfumo wa jamii wa kuendesha masuala yake. Siasa inaweza kuwa itikadi inayofuatwa na kundi au jamii fulani ambayo ndiyo msingi wa kuendesha uchumi, utamaduni na mwenendo mzima wa maisha ya jamii husika (TUKI, 2004). Siasa ni hali ya raia yeyote yule ya kujihusisha na mchakato wa kuhakikisha kwamba masilahi ya jamii nzima yanazingatiwa.

### **Kiswahili na Ukuzaji wa Demokrasia**

Kuna njia nyingi za kukishirikisha Kiswahili katika shughuli za demokrasia. Siasa bila lugha haipo, lakini lugha inaweza kuwepo bila kutegemea siasa. Demokrasia kama tulivyosema ni mfumo fulani wa siasa. Ili pawepo na siasa zinazozingatia demokrasia, ni lazima kanuni na sheria zinazozingatia mfumo huu ziandikwe katika katiba ya taifa. Katiba ni waraka ambao husheheni kanuni, njia au mwongozo unaotumiwa na nchi au kundi fulani katika kuendesha shughuli za kila siku. Hiki ni chombo muhimu cha kuendeleza demokrasia kuliko waraka mwingine ule wa kitaifa. Ni kutokana na katiba ambapo wananchi hupata haki zao. Pia, maelewano baina ya mwananchi na viongozi kuhusu jinsi ya kutawaliwa hufafanuliwa. Vilevile, mwananchi wa kawaida hupata fursa ya kujifahamisha jukumu lake na kutoa mchango wa kujenga nchi (Njogu, 2007: ix). Demokrasia haiwezi kujengwa bila kuwashirikisha wananchi moja kwa moja. Kauli muhimu sana katika demokrasia ni kuzingatia uamuzi wa wengi huku hoja za wachache zikisikilizwa.

Akizungumzia hili, Njogu (keshatajwa) anasema, matumizi ya Kiswahili katika taasisi za umma na za kibinafsi hayajashika kasi nchini Kenya kama inavyotakiwa. Hata hivyo, hali hii inatazamiwa kubadilika kutokana na kuzinduliwa kwa katiba iliyoanza kutekelezwa tarehe 4/8/2010. Katika katiba hii mpya, hadhi ya lugha ya Kiswahili imeinuliwa kwa kupewa uwezo wa kutumika kama lugha rasmi. Hatua hii imekiweka Kiswahili katika hali sambamba na Kiingereza. Hata hivyo, mengi yanahitajika kufanywa ili kukiwezesha Kiswahili kutumika kikamilifu katika kuendesha shughuli za kiofisi kwa njia sawa na lugha ya Kiingereza ambayo imetumika miaka mingi. Licha ya katiba ya nchi kutaja nafasi ya Kiswahili, inapaswa pia kunakiliwa katika Kiswahili ili kumwezesha mwananchi wa kawaida kuing'amua barabara. Nchini Kenya, ilikuwa hatua muhimu kwa kuchapisha kwa Kiswahili nakala za kielelezo cha katiba iliyopendekezwa na kupitishwa mwezi Agosti mwaka 2010. Hatua hii imechangia katika kuinua kiwango cha uelewa wa haki wa mwananchi wa kawaida pamoja na uelewa wa mfumo wa serikali. Pia, mwananchi ameelewa vyema haki zake za kimsingi kwa sababu anazisoma kwa urahisi katika katiba ya taifa iliyoandikwa kwa Kiswahili. Hali hii imefanya serikali kutambua nguvu na uwezo wa wananchi. Ni kutokana na hali hii ambapo mahojiano ya kuajiri watakaoshikilia nyadhifa za kiserikali yanafanyika hadharani huku yakihusisha wananchi wa kawaida

ambao huruhusiwa kutumia Kiswahili katika kuchangia maoni yao kuhusu wanaonua kupewa nyadhifa za juu serikalini. Hii ni hatua kubwa ya kuendeleza demokrasia. Ni katika mwelekeo sawa na huu ambapo nyaraka zingine muhimu za kitaifa zinafaa ziandikwe katika Kiswahili na kisha lugha za kigeni.

Kunakili nyaraka kama vile katiba, sheria zinazoundwa na wabunge (*Act of Parliament*) pamoja na maongozi ya serikali katika Kiswahili kutatoa nafasi kwa mwananchi ambaye umahiri wake wa lugha za kigeni ni mdogo au haupo, kuzielewa bila tatizo kubwa. Hivyo basi, kila mtu kuanzia ngazi ya chini hadi ya juu, ataweza kubainisha na pia kuelewa kwa undani maongozi ya serikali yake. Hatua kama hii itampa mwananchi uwezo wa kutetea haki zake na za wenziwe. Mwananchi wa aina hii atashiriki kikamilifu katika uundaji wa mfumo wa utawala wenye kuzingatia usawa na haki. Kitendo cha kunakili nyaraka muhimu za kitaifa katika Kiswahili, katika mazingira ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini kinaweza kulinganishwa na hatua iliyochukuliwa na Wamishonari wa Kikristo ya kutafsiri Bibilia takatifu katika lugha za kiasili. Hatua hii iliwasaidia wamishonari kueneza injili. Vivyo hivyo, wanademokrasia wa kila nchi husika wanapaswa kupigania nyaraka muhimu za nchi ziandikwe kwa Kiswahili ili umma upate kuzielewa kwa urahisi. Isitoshe, wanademokrasia wana jukumu kubwa la kuhakikisha kwamba katiba ya nchi inafafanua sera ya lugha katika nchi husika. Katika sera ya lugha, inawabidi wanaharakati wa demokrasia kutetea kujumuishwa njia za kustawisha lugha za kiasili kikiwemo Kiswahili. La si hivyo demokrasia asilia ya Waafrika haitanawiri kwa sababu itakuwa imeathiriwa na lugha za kigeni.

Utandawazi una sura mbili, yaani sura njema na mbaya. Sura mbaya ya utandawazi inaleta hofu kiasi kwamba watu wengi wanatamani kuwa na kitu asilia kilicho na uwezo wa kuhimili imani na maadili ambayo hayajaingiliwa na uhayawani (Njogu, 2007: x). Kitu hicho chenye kusheheni utu huu ni Kiswahili, hasa katika mazingira ya Afrika Mashariki, Kati na Kusini, na ikiwezekana bara zima la Afrika. Kinachohitajika ili kufikia lengo hili, ni kwamba, wataalamu wa lugha pamoja na wanasiasa wanapaswa kujua kwamba wao ni vyombo muhimu vinavyoweza kulielekeza bara hili katika mkondo unaofaa ili wajikinge na msukumo unaotokana na athari mbaya za utandawazi. Wasomi na wanasiasa ndio watakaopromosha demokrasia kwa kuendelea kutumia lugha za kigeni ambazo zina athari kubwa ya ukandamizaji. Vivyohivyo, wanaweza kukuza demokrasia kwa kukuza na kuendeleza lugha za kiasili. Kiswahili ni lugha ya kiasili kwa sababu chimbuko lake linapatikana nchini Kenya. Katika hali hii, Kiswahili ni lugha yenye uwezo mkubwa wa kuendeleza demokrasia huku ikisaidia kukabiliana na athari za utandawazi.

Katika tawala nyingi za jadi za jamii za Kenya, mfumo wa utawala uliozingatiwa ulihusisha wazee pakubwa. Wazee hawa walihakikisha kwamba maoni ya watawaliwa yanazingatiwa. Dhana ya imla ilitokana na majilio ya wageni ambao walileta ubinafsi na hali ya kutaka kukalia na kudhibiti wengine; yaani ukoloni-mkongwe na ukoloni-mamboleo, ambayo ni mifumo ya kiimla. Kutokana na fasihi simulizi ya jamii nyingi za Kiafrika, hakujawahi kutajwa jamii fulani katika enzi za zamani ambayo iliwahi

kukalia nyingine kimabavu, ama mzee fulani ambaye ni kiongozi katika baraza la wazee aliyewashurutisha wengine kukubaliana na uamuzi ambao ungetia raia wa jamii yake katika hatari kwa misingi kwamba yeye ni wa cheo cha juu kuzidi wengine. Hii ndiyo sababu iliyowafanya wahenga hawa kuwa na methali kama, “Umoja ni nguvu na utengano ni udhaifu”, “Mgalla muue na haki umpe”, “Wengi wape, usipowapa watachukua”, “Asiye kubali kushindwa si mshindani” “Penye wazee hapaharibiki neno” na nyingine nyingi ambazo zilitaja masuala ya haki na umoja wa Waafrika. Itakuwa vyema na bora ikiwa lugha ya Kiswahili inayosheheni misemo mingi yenye kukuza demokrasia itatumika hususan enzi hizi za utandawazi.

Tuchukulie mfano wa baraza la wazee katika jamii ya Wameru nchini Kenya, ambalo linajulikana kwa jina *Njuri-ncheke*. Baraza hili hushikilia na kuendeleza mila, desturi na mbeko za jamii pana ya Wameru. Ni maarufu sana katika kutatua mizozo ya kieneo, kesi za mashamba na za kijamii bila mapendeleo. Pia, hutoa mwelekeo fulani katika masuala ya uongozi katika jamii ya Wameru, japo mara kwa mara huingiliwa na wanasiasa – tabia ambayo ni ya kigeni inayochangia udikteta. Hata hivyo, baraza hili huweza kukubaliana na ushawishi wa wanasiasa wenye ubinafsi na hatimaye kudumisha usawa na haki katika vikao vyake. Katika vikao hivi, lugha rasmi ni Kimeru na wakati mwingine wazee hawa hutumia Kiswahili kuhakikisha haki ikiwa wana mgeni au mhusika asiye fahamu Kimeru. Matumizi ya Kiswahili katika vikao vya baraza hili huwa ni kwa nia ya kufanikisha mawasiliano baina ya wageni na wazee wa Kimeru. Katika hali hii, Kiswahili huwa chombo madhubuti cha kuendeleza utawala bora. Mwingiliano wa namna hii ambao hufanikishwa na Kiswahili ni kipengele muhimu cha utandawazi. Wazee hawa wanaowakilisha kila sehemu ya eneo kuu la Meru, hawana budi kuendesha mijadala yao kwa lahaja tofauti za Kimeru na wakati mwingine hutumia Kiswahili. Je, demokrasia lazima itazamwe kwa jicho la kigeni ili iafiki maana? Kwa kweli serikali kuu ya Kenya imelazimika wakati mwingi kuitisha usaidizi wa baraza la Njuri Ncheke ili kutatua mizozo inayotokana na mipaka ya kiutawala iliyowekwa na mkoloni. Zamani, na hata leo, wazee hawa kwa kutumia lugha yao ya kiasili, waliweza kuketi chini na kusawazisha masuala mengi yaliyoleta utata. Kwa mfano walishughulikia suala la mahari ambalo lilihusisha kuweka idadi mwafaka ya mifugo inayopaswa kulipiwa mwanamwari kutoka jamii tofauti za Wameru. Aidha, walitoa mwongozo kuhusu biashara ya kubadilishana bidhaa kwa bidhaa.

Lugha ndicho chombo kinachosaidia watu kujitambulisha na kujinasibisha na hali fulani, eneo, ukoo na nchi. Marshad (1993) anashadidia sababu ya kujitambulisha anaposema kuwa tabia moja ya binadamu ni kupenda kujifahari kwa jina la taifa lake. Zamani, wanajamii walijinasibisha na mababu zao au kabila lao. Leo, hali hii imebadilika na kuchukua mwelekeo mwingine ambapo imepata sifa ya kiwango cha juu kiasi kwamba aghalabu mwanajamii hujinasibisha na nchi yake. Hivi ni kusema kwamba kitambulisho pamoja na hali ya kujinasibisha na kitu fulani kama taifa ni suala muhimu katika aushi ya binadamu yeyote yule. Lugha ndiyo msimbo unaobeba kitambulisho cha mtu katika ngazi ya juu, ikifuatiwa na utamaduni wa mtu huyo.

Lugha za kiasili zinatekeleza dhima ya utambulisho katika kima cha chini ambacho ni cha kiukoo. Kiswahili ni kitambulisho katika kima cha juu ambacho ni cha kitaifa na kikanda. Ili kuondoa athari za ukabila, ambazo zimekuwa dondandugu nchini Kenya, suala la lugha ni muhimu litiliwe maanani. Ukabila ni kikwazo kikubwa cha utandawazi na demokrasia katika kiwango cha kitaifa. Katika hali hii, lugha ya Kiswahili ina wajibu wa kuendeleza demokrasia na utandawazi nchini Kenya kwa kiwango cha juu kwa kuondoa athari za ukabila zinazochangiwa pakubwa na hali ya raia kujinasibisha na lugha zao za kiasili.

Hata hivyo, uwingilugha katika taifa si tishio la umoja wa nchi kama wengi wanavyofikiria. Mgawanyiko wa nchi hutokana na mambo kama vile ubinafsi, ubaguzi, ufasidi, sheria dhalimu na uongozi mbaya. Kuna nchi kadha zinazotumia lugha moja lakini zimesambaratika. Mfano ni nchi ya Somalia inayomilikiwa na asilimia kubwa na raia wa Kisomali na kwa ujumla watu wote hutumia lugha ya Kisomali. Nchi hii imekuwa katika vita kwa muda wa zaidi ya miaka thelathini kutokana na ubinafsi wa viongozi wake. Uwingilugha unaweza kulinganishwa na urithi ambao umerithishwa watoto kadhaa wa familia moja baada ya kifo cha wazazi wao. Kisha wana wa wazazi wendazao wakashindwa kufaidi mali ile, kwa sababu mali hiyo ni adhimu na ikawazidishia majivuno na kuwafanya wapotoke. Hivyo ndivyo ilivyo katika nchi ya Kenya, ambayo ina utajiri mwingi wa lugha; kwa hivyo, Wakenya wana hiari ya katumia lugha hizi kama hazina ya taifa ya kuwaletea fahari au vyombo vya kuleta maangamizi kati yao. Wakenya wanapaswa wahamashishwe ili waelewe kwamba Kiswahili ni lugha sambazi ambayo inaweza kusawazisha mawasiliano katika mazingira ya uwingilugha; hivyo, kufanikisha demokrasia ambayo ni athari nzuri ya utandawazi. Kiswahili kinaweza kuwa kitambulisho sawazishi kati ya waneni wa lugha za kiasili na kwa njia moja au nyingine kikasaidia kulinda Wakenya dhidi ya athari zisizofaa za utandawazi ambazo huenda zikaletwa na lugha na utamaduni wa kigeni.

### **Nafasi ya Kiswahili katika Ujenzi wa Demokrasia**

Kiswahili ni lugha ya Kiafrika ambayo imepanuka na kuenea katika sehemu nyingi za dunia. Ni lugha sambazi katika Afrika Mashariki, Kati na Kusini; mataifa ya Jumuiya ya Afrika Mashariki yameitambua kama lugha ya jumuiya na vilevile Muungano wa Afrika. Kutokana na hali hii, imekumbatiwa na nchi ya Uganda na Rwanda kama lugha rasmi tofauti na hali ilivyokuwa hapo awali (Chimerah, 1998; Mukuthuria, 2006). Inatazamiwa kwamba nchi zote zinazojiunga na jumuiya hii ikiwemo Sudani ya Kusini iliyojiunga juzi na zingine zitakazojiunga siku za baadaye zitatoa kauli na msimamo thabiti kuhusu lugha ya Kiswahili. Licha ya umuhimu wa lugha hii katika mazingira ya Afrika, pia, inatumika katika mataifa mengine yasiyo ya Afrika. Mifano ni kwamba, Kiswahili kinafunzwa kama somo katika vyo vikiu takribani mia moja nchini Marekani; aidha, inafunzwa kwingineko ulimwenguni (Chimerah, 1988; Mukuthuria, 2006; Mukuthuria, 2009). Katika, nchi ya Oman, theluthi moja ya idadi ya watu hutumia Kiswahili kama lugha ya kwanza. Wazungumzaji hawa ni wale waliotoka Zanzibar na kurudi Oman kutafuta mababu zao wa Kiarabu (Chimerah, keshatajwa).



Kwa hivyo, ni bora kukitumia Kiswahili ili kujenga demokrasia badala ya lugha za kigeni ambazo zimesheheni utamaduni wa Kimagharibi uliosambaa kwa kasi kutokana na msukumo wa utandawazi. Kwingineko, Kiswahili kina athari chache ya ukoloni. Lugha zote ambazo wakoloni walizitumia zinanasisibishwa na hali ya utwana na ubwana. Lugha za kigeni zimewafanya viongozi Waafrika kuhisi kuwa lazima wao pia watawale kwa mabavu kama walivyofanya wabeberu. Kwa kweli lugha za viongozi hawa ni zile za wakoloni. Jambo hili linaondoa usawa baina ya wanajamii; hivyo basi kuitinga demokrasia. Kwa njia nyingine, lugha za kigeni licha ya kuwa zimetokea kwenye mataifa ambayo yanapigania demokrasia, zinawafanya Waafrika kuuchukia Uafrika wao. Hii ni athari mbaya ya utandawazi inayoletwa na wafuasi walio na mielekeo ya kupendelea lugha za kigeni.

Kwa upande wa Kiswahili, hii ni lugha ya Kiafrika. Wazungumzaji wa Kiswahili wanafahamu fika kuwa hii ni lugha yenye usawa; ni lugha yenye msingi mwema wa kujenga utaiifa. Kielelezo kizuri cha taifa la Kiafrika lililojenga demokrasia na utaiifa kwa kutumia Kiswahili ni nchi ya Tanzania. Njogu (2007) amesema kuwa mara kwa mara, Wakenya wameonyesha kupendezwa na juhudi zilizofanywa na Mwalimu Julius Nyerere za kujenga hisia za utaiifa nchini Tanzania. Uongozi wa Nyerere ulitoa kauli kuwa Kiswahili ndiyo lugha ya taifa na baadaye lugha ya kufundisha shuleni. Mikutano yote ya hadhara ilifanywa kwa Kiswahili. Falsafa ya sera shirikishi ilihitaji matumizi ya lugha ya Kiswahili. Maoni haya yanaonyesha kuwa Kiswahili ni chombo muhimu katika kujenga mfumo imara wa siasa katika nchi za Afrika Mashariki, Kati na ikiwezekana Afrika nzima.

Kuimarika kwa demokrasia kunaenda sambamba na mabadiliko ya kiuchumi na kiutamaduni. Nchi za Afrika Mashariki na Kati zinafaa kutumia lugha yenye asili ya Kiafrika katika kuandaa mikakati ya kuukarabati na kuudhibiti utamaduni wao. Katika hali hii, utamaduni unaofaa kuundwa ni ule ambao utakidhi mahitaji ya kisiasa, kiuchumi na kijamii. Hii ni kwa sababu utamaduni wa nchi husika unatishiwa na mwingilio wa mitindo ya kigeni ambayo inasababishwa na utandawazi. Kwa mfano, baadhi ya mikakati ya kuukarabati utamaduni nchini Kenya inafaa kuhusisha matumizi ya lugha inayoeleweka na Wakenya walio wengi. Kwa kufanya hivi, Wakenya wataweza kujikinga dhidi ya athari mbaya za utandawazi ambazo zinatishia utamaduni wao. Suala hili la kutumia Kiswahili ili kujenga utamaduni dhabiti nchini Kenya limeungwa mkono na wanazuoni wengi. Kwa mfano, Chris Wanjala amenukuliwa na gazeti la *East Africa Standard*, (Agosti 10, 2007) akisema kwamba kuna haja ya Afrika kujikomboa kutoka kwa minyororo ya lugha na ukadamizwaji wa kiutamaduni ambao umewekwa na mabwana wa kikoloni na badala yake kuwe na lugha ya Kiafrika ya kutumika katika majukwaa ya kimataifa. Lugha hii ni Kiswahili. Msomi maarufu wa Kiafrika, Wole Soyinka, alipozuru nchi ya Kenya mwaka 2009, pia aliunga rai hii mkono.

### **Mfumo wa Mahakama na Demokrasia**

Aidha, demokrasia huhitaji mfumo wa mahakama ambao hausepetuki. Mahakama imara zinazohudumia wananchi pasipo kuzingatia hadhi au cheo cha mshtakiwa ama

mlalamishi. Haki hupatikana mahakamani kiasi kwamba, ukweli hutenganishwa na uongo. Nchini Kenya, lugha rasmi ya mahakama ni Kiingereza, kwa sababu hiyo, watu ambao hawana weledi wa Kiingereza hushindwa kujitetea, ama kuwasilisha malalamiko yao. Mashahidi huwa hawatoi ushahidi kikamilifu. Kikundi cha watu kama hawa hunyimwa haki zao za kisheria, hatua ambayo inaangazia demokrasia. Tatizo hili linaweza kukabiliwa ikiwa nchi ya Kenya itatumia Kiswahili katika kuendesha shughuli za korti. Wananchi wa kawaida (ambao si wanasheria) wataepukana na hali ya kutengwa. Istilahi za lugha katika muhtadha wa mahakama ni ngumu hasa ikitokea kwamba etimolojia yake huwa ni lugha za nchi zilizokuwa koloni za Afrika. Kwa mfano msamiati - *Nor Prosquete* - kuachiliwa huru kwa kukosa ushahidi; *Plaintiff*-mlalamishi na istilahi zingine zenye asili ya kilatini ilikochota sana sajili ya sheria ni baadhi ya maneno ambayo hayawezi kueleweka na raia asiye mtaalamu wa sheria. Katika hali hii, Kiswahili kikitumiwa na wanasheria kutoa fasili na ufafanuzi wa sheria kwa wananchi, sheria za nchi zitaeleweka vyema. Mwakili mara nyingi huandaa warsha kuhusu sheria ambapo wanaoshiriki ni watu ambao wengi wao hawana weledi wa kisheria. Vikao hivi vitakuwa na manufaa zaidi iwapo lugha ya fasili ni Kiswahili. Isitoshe, watumishi wa umma kama vile machifu, makamishina wa kaunti na magavana wanapaswa kutumia Kiswahili wakati wa kutoa maelezo ya kisheria, hususan sheria za bunge kwenye mabaraza ya wanavijiji. Ni katika hali hii ambapo taaluma ya tafsiri itahitajika ili kufanikisha mawasiliano. Akizungumzia tafsiri, Mukuthuria (2007:121) anasema kwamba, ingefaa tuyaone manufaa inayopata lugha kutokana na shughuli ya kutafsiri kama matokeo ama athari zinazoibuka katika jitihada za kufanikisha mawasiliano. Cha muhimu hapa, ni manufaa yanayopatikana katika demokrasia baada ya kutafsiri na kufasili sheria kwa kutumia Kiswahili. Kinachofaa kutiliwa nguvu hapa ni kwamba Kiswahili kinafaa kutumika kutoa tafsiri ya dhana za kigeni kuhusu sheria za taifa na kimataifa ambazo zinaletwa na utandawazi. Kwa kufanya hivi sheria hizi zitaafiki mtazamo wa dunia wa Wakenya na Waafrika kwa jumla.

### **Kampeni**

Aidha, matumizi ya Kiswahili katika mikutano ya kisiasa yanaweza kuleta mwelekeo chanya kuhusu demokrasia. Wanasiasa hasa katika nchi yenye vyama vingi kama Kenya, wanapaswa kuwashirikisha wafuasi wao katika kuzielewa shughuli za serikali na harakati za wanamageuzi katika mataifa mengine. Hii ni kwa sababu dunia imekuwa kijiji, na hivyo, mabadiliko ya kisiasa katika nchi moja yanaweza kuathiri nchi nyingine hata ikiwa nchi hizo si majirani. Ni katika mikutano ya hadhara ambapo wapigaji kura nchini Kenya wanapaswa kujulishwa dhima na wajibu wao katika kukuza mfumo bora wa utawala. Wanapaswa kuhamasishwa ili wadai haki zao kama inavyofanyika katika mataifa mengine. Je wanasiasa wakitumia lugha ambayo haieleweki na kila mtu, wafuasi wao watanufaika kwa njia yeyote? Ni muhimu watumie Kiswahili ambacho ni chombo asilia na tena lugha sambazi isiyo na mwelekeo wa mabwana na watumishi. Tatizo lililopo nchini Kenya ni kwamba baadhi ya wanasiasa hawakimudu Kiswahili. Hali hii huchangia kukwamiza mawasiliano baina yao na wananchi. Kwa hivyo, pamoja na kuendesha kampeni kwa lugha ya

Kiswahili, kule kuchanganya Kiswahili na lugha za kiasili kunakosesha Kiswahili hadhi kinayostahiki kama lugha rasmi na lugha ya taifa Kenya.

### **Shughuli za Tume ya Uchaguzi**

Tume ya Uchaguzi ni chombo muhimu katika kukuza demokrasia. Ni taasisi ambayo yapaswa kuwa huru kutoka kwa ushawishi wa wanasiasa. Ni taasisi iliyo na jukumu la kuwaelimisha wapiga kura jinsi ya kushiriki katika shughuli za uchaguzi. Kadhia za udanganyifu na uharibifu wa kura hazipaswi kutokea katika chaguzi za kitaifa. Matukio kama haya ni hatari na tishio kubwa la demokrasia. Pia, yanaweza kusababisha umwagikaji wa damu kama ilivyoshuhudiwa nchini Kenya mwaka wa 2007/2008. Ni wajibu wa Tume ya Uchaguzi kuendesha uchaguzi kwa njia iliyo huru na yenye haki katika viwango vya vyama vya kisiasa mashinani na katika kiwango cha kitaifa. Hatimaye inatakiwa kutangaza matokeo jinsi yalivyo bila kupanguliwa. Mafanikio ya mawasilino baina ya wapiga kura na Tume ya Uchaguzi hutegemea matumizi ya lugha inayogusa hisia na kufikirisha wapiga kura kiasi kwamba watatafakari kwa kina kabla ya kuwachagua viongozi. Lugha kama hii haipaswi kuegemea kwenye misingi ya kikabila. Inapaswa kuwa lugha itakayowasaidia wapiga kura kuwa na macho yanayotazama mambo kwa undani na uzalendo zaidi ili kuuona ukweli wala si ukabila au umaeneo. Pana haja ya mafisaa wa tume kutumia Kiswahili badala ya lugha za kigeni ambazo zinatenga raia wasiozielewa. Matumizi ya lugha za kigeni husababisha wananchi kutumia lugha za kiasili wanapojadili shughuli za uchaguzi ili kufidia upungufu wa mawasiliano. Hali hii ya kutumia lugha za kiasili hufungamanishwa kimakosa na dhana potovu ya ukabila. Kulingana na jinsi hali ilivyo, dhana ikishaingia katika jamii, iwe potovu au nzuri ni vigumu kuiondoa.

Wakati huohuo, tume itafanikiwa zaidi iwapo itaendesha vikao vyote vya elimu ya raia kuhusu uchaguzi kwa Kiswahili. Hali halisi ni kwamba hakuna elimu ya raia kuhusu uchaguzi inayofanywa kwenye vikao vya umma. Kinachofanyika ni kubandikwa kwa mabango yaliyoandikwa kwa lugha mbili ambazo ni Kiswahili na Kiingereza. Mabango haya hayatoi mchango mkubwa kwa sababu kuna baadhi ya wananchi wasiojua kusoma na kuandika. Matumizi ya Kiswahili ni muhimu kwa sababu kuna istilahi nyingi ambazo ni za kiufundi zisizoeleweka kwa urahisi katika lugha ya Kiingereza. Mfano wa maneno haya ni:

<b>Kiingereza</b>	<b>Kiswahili</b>
<i>Rigging</i>	udanganyifu
<i>Petition</i>	malalamiko
<i>Referendum</i>	kura ya maoni

Mashirika ya kutetea haki, mageuzi na uhuru yanayo thamana ya kuendeleza demokrasia kwa ushirikiano na tume ya uchaguzi. Makundi haya yatafanikiwa zaidi iwapo yatumia Kiswahili. Mwananchi wa ngazi ya nchi atashirikishwa ipasavyo katika vuvuvugu la kudai demokrasia iwapo mawasiliano baina yao ni laini. Rai hii inaungwa mkono na Njogu (2007) anaposema kuwa chama cha CHAKITA kimetia juhudi katika kuhakikisha kwamba suala la lugha limetiwa katika mazungumzo ya

kitaiifa. Anaendelea kusema, kuna imani kwamba ni muhimu kuwahusisha wananchi wa kawaida katika harakati za kubadilisha mfumo wa kiuchumi na kisiasa. Hivi ni kusema kwamba wananchi wanapaswa kushirikishwa katika mchakato mzima kwa kutumia lugha wanayoielewa vizuri. La si hivyo, athari hasi za utandawazi zitaingilia mfumo mzima wa kisiasa, kiuchumi na kitamaduni kupitia matumizi ya lugha ya kigeni.

### **Nafasi ya Fasihi ya Kiswahili**

Wasanii wana jukumu kubwa la kuwazindua wanajamii kwa kumulika maovu ama maendeleo ya jamii. Mojawapo ya matokeo ya umilikaji wa maovu ya jamii ni kushtumu na kukejeli mfumo wa utawala wa kiimla. Kwa kufanya hivi jamii ya kimataifa pia huweza kujua yanayojiri katika nchi husika. Uzinduzi kutokana na wasanii utafaulu zaidi iwapo watumia lugha ambayo haifungamanishwi na historia ya unyanyasaji wa wenyeji wa nchi husika. Inaeleweka kwamba msanii huteua maneno fulani ya lugha mahususi na kisha kuyafinyanga ili kuwasiliana na hadhira yake (Senkoro, 1982). Katika harakati za kusaka uhuru, haki na usawa, cha muhimu ni kuleta mabadiliko katika mfumo mzima. Mabadiliko yanapaswa kuhusisha matumizi ya lugha ambayo wanaonyanyaswa watajinasibisha nayo. Jambo hili ni muhimu ili kuleta mshikamano na umoja baina ya umma unaopigania demokrasia. Mfano mzuri ni matumizi ya Kiswahili na Waafrika katika harakati za kumpiga vita mkoloni. Leo, lugha ya Kiswahili inaweza kutumiwa na wasanii kama ngao ya kuingia demokrasia na pia silaha ya kupigania haki, usawa na utawala bora kwa jumla. Pia, kazi ya wasanii ni muhimu katika kupitisha mawazo ya Wakenya katika ulingo wa kimataifa. Hii ni kwa sababu hali hii husaidia kuwapa Wakenya nafasi ya kuchangia utandawazi hususan katika mitindo ya nyimbo. Tawala nyingi zinazotinga demokrasia barani Afrika hutumia lugha za kikoloni. Fasihi inayokubaliwa na viongozi wa kiimla huwa haikejeli wala kusuta utawala mwovu. Kwa hivyo, ni jambo la manufaa kwa Wakenya wakati wasanii wanapotumia Kiswahili kutetea na kuhamasisha demokrasia katika kazi zao za kisanaa. Mfano wa fasihi kwa Kiswahili inayoendeleza demokrasia inaweza kupatikana katika baadhi ya vitabu kama vile: *Kilio Cha Haki* cha Al-Amin Mazrui(1981), *Mafuta* cha Katama Mkangi(1984), *Kifo Kisimani* cha Kithaka wa Mberia(2001), *Dunia Mti Mkavu* cha Said A. Mohamed(1980) na nyingine nyingi. Kazi hizi huhamasisha wananchi wengi kwa sababu hulenga hadhira kubwa kuliko fasihi iliyoandikwa kwa Kiingereza au lugha nyingine yoyote ambayo ni ya kigeni.

### **Vyombo vya Habari na Demokrasia**

Katika ulimwengu wa kisasa, utawala hauwezi kujitenga na vyombo vya habari. Wanahabari ni macho ya umma. Vyombo hivi hutekeleza dhima ya kuwa macho ya umma kwa idhini au bila idhini ya serikali. Vyombo vya habari vinayo nafasi kubwa ya kueneza habari za utawala bora ama kushtumu mfumo dhalimu. Kupitia vyombo hivi, magwiji wa taaluma ya sayansi ya siasa na watu wengine hutoa maoni yao kuhusu mfumo wa utawala. Mara nyingi maoni kama haya nchini Kenya huchapishwa katika magazeti yanayotumia lugha za kigeni. Kwa mfano, maoni mbalimbali kuhusu siasa

hupewa uzito katika magazeti ya *Daily Nation* na *East Africa Standard* yanayotumia lugha ya Kiingereza wala si katika gazeti la “Taifa Leo” linalotumia lugha ya Kiswahili. Gazeti la Taifa leo ndilo gazeti pekee la lugha ya Kiswahili nchini Kenya. Hata hivyo, gazeti hili limepuuzwa na watu wengi kwa sababu habari zinazochapishwa zikihusiana na siasa na utawala hazipewi uzito kama ilivyo katika gazeti dada la *Daily Nation*. Aidha, Gazeti lenyewe lina kurasa chache likilinganishwa na mengine ya Kiingereza. Pia, masuala yanayowavutia wasomaji wa magazeti kama vile habari kuhusu biashara, nafasi za kazi, burudani na mitindo mbalimbali ya maisha hayapo. Kwa hivyo, wakati mwingi huwa hakuna kichocho cha kuwafanya watu wengi kusoma gazeti la Taifa Leo nchini Kenya. Hali hii imechangia kwa njia moja au nyingine kuwanyima wananchi wasiokuwa na weledi wa Kiingereza kupata na kufahamu kwa ukamilifu yanayojiri katika uwanja wa siasa na pia nyanja nyingine za maisha. Katika hali hii, athari za utandawazi kuhusu siasa, uchumi na utamaduni; ziwe nzuri au mbaya huingizwa nchini Kenya kupitia vyombo vya habari vinavyotumia Kiingereza.

Mashirika ya utangazaji yana uwezo mkubwa wa kutoa mchango wa kuendeleza demokrasia na wakati huo yakichuja athari mbaya za kisiasa zinazoletwa na utandawazi. Stesheni za redio zinapaswa kutangaza matukio na maoni ya wanasiasa kwa kutumia lugha ya taifa – Kiswahili. Dhima hii inapaswa kutekelezwa zaidi na idhaa zinazotangaza kwa kutumia Kiswahili nchini Kenya na nje ya Kenya. Hii ni kwa sababu kuna redio kadha ulimwenguni ambazo zinatumia Kiswahili kama mojawapo ya lugha za utangazaji na husikilizwa na Wakenya. Baadhi ya idhaa hizi ni: Redio Moscow, Redio China Kimataifa, Shirika la Utangazaji la Uingereza (BBC) London, *Channel of Afrika* – Afrika Kusini, Sauti ya Amerika (VOA) Washington DC, Redio Rwanda – Kigali, Redio Burundi – Bunjumbura, Redio Deutche – Welle – Cologne Ujerumani (Mazrui na Mazrui, 1995; Chimera, 1998; Mukuthuria, 2006; 2009).

Ukandamizwaji wa demokrasia nchini Kenya ulishuhudiwa miaka ya 1980 na 1990 ambapo kulikuwa na redio na runinga moja iliyomilikiwa na serikali. Wananchi walinyimwa haki na hawakupata habari zilizohusiana na serikali, hasa za maovu na dhuluma zilizoendeshwa wakati huo. Katika kipindi hiki hakuna mwanasiasa yeyote angedhubutu kupinga serikali wala kuikosoa hadharani kupitia redio ama runinga ya taifa. Ni katika hali hii ambapo wanasiasa wa Kenya waliotaka mageuzi walitafuta njia mbadala ya kutoa maoni yao kuhusu demokrasia. Aidha, wanaharakati wa demokrasia walitumia vituo vya habari vya kigeni vilivyokuwa vinapeperusha matangazo kwa Kiswahili kuwatia wananchi ari ya kutaka mageuzi. Vituo vya redio vya BBC na Redio Dautche-Welle vilitekeleza wajibu mkubwa wa kuwajuvya Wakenya yaliyokuwa yakijiri nchini mwao. Mateso, mauaji na kukiukwa kwa haki zingine za kibinadamu kuliangaziwa sana na vyombo hivi vya habari ambavyo vilitenga muda fulani wa kuangazia masuala ya Afrika kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Katika enzi hizo, ikifika mwendo wa saa 12:30 jioni, wananchi wapenda mageuzi walikuwa wanazingira redio moja katika kijiji ili wapate habari ‘sahihi’ kuhusu harakati za kudai demokrasia. Habari hizi zilipeperushwa kwa Kiswahili na shirika la BBC kutoka Uingereza. Hata

hivyo, hali ni tofauti hii leo kwa sababu, ijapo uhuru wa vyombo vya habari unakandamizwa, Wakenya wanaweza kupata habari kupitia mfumo mpya wa kidijitali wa kupeperusha habari. Katika mfumo huu, ni rahisi kupata habari sahihi kuhusu Kenya kutoka mashirika ya habari ya kimataifa kama vile Al Jazeera na CNN. Habari hizi huwafikia Wakenya licha ya serikali kuificha. Hii ni athari chanya ya utandawazi na maendeleo makubwa kwa demokrasia ambayo yalifanikishwa na matumizi ya lugha ya Kiswahili kupitia idhaa za kigeni. Tangu wakati huo, vituo kadha vya redio na runinga vinavyopeperusha matangazo kwa Kiswahili vimeanzishwa. Idhaa kama vile Redio *Citizen*, Redio Jambo, Kiu FM, Redio Maisha na Milele *FM* hutumia Kiswahili pekee katika kurushia matangazo. Kwa kweli idhaa hizi na nyingine zimechangia pakubwa katika kuendeleza demokrasia nchini Kenya. Vituo hivi vilitekeleza wajibu mkubwa wa kuwafafanulia wananchi pendekezo la katiba mpya ambayo hatimaye ilipitishwa. Fauka ya hayo, vyombo vya habari vinatekeleza wajibu mkubwa katika kuhakikisha katiba mpya inatekelezwa ipasavyo. Vinapeperusha moja kwa moja mahojiano ya kazi kuhusu nyadhifa kuu za umma kama vile wadhifa wa jaji mkuu, majaji wa mahakama ya juu, makamishina wa tume huru ya uchaguzi na mipaka.

Vilevile, vyombo vya habari nchini Kenya vina thamani ya kurusha hewani majadiliano ya bunge la taifa. Bunge la taifa kama taasisi muhimu ya kuendeleza demokrasia linapaswa kutumia lugha ya Kiswahili wakati wa kujadili hoja. Vyombo vya habari navyo vinapaswa kupeperusha majadiliano moja kwa moja kutoka jengo la bunge. Changamoto ambayo imekuwepo nchini Kenya ni kuwa sheria za nchi hazikuweza kuruhusu matangazo kupeperushwa moja kwa moja kutoka bungeni. Hata hivyo, ingawa sheria zimebadilishwa kuruhusu kupeperushwa mijadala ya wabunge moja kwa moja, kuna wabunge wengi ambao hawawezi kukimudu Kiswahili, ama wanakidunisha. Wabunge kama hawa wameathiriwa na kasumba ya kikoloni na ingefaa zaidi kama wangebadi mwelekeo wao kuhusu Kiswahili na kukitumia bungeni. Kwa kufanya hivi hoja zinazojadiliwa; ziwe za kitaifa au kimataifa ambazo ni za kitandawazi zingewafikia Wakenya kwa urahisi.

### Hitimisho

Makala hii inapendekeza kwamba ukuzaji wa demokrasia uanzie mashinani na ushirikishe wananchi wote kwa kutumia lugha ya Kiswahili. Aidha, sera mwafaka ya lugha itungwe ili kuondoa hali ya kuchanganyikiwa baina ya upanuzi wa Kiswahili na matumizi ya Kiingereza ambayo imetumika kama lugha rasmi kwa muda mrefu. Pia, makala hii inapendekeza vyo vya vikuu na vya kadiri nchini Kenya vianzishe mafunzo ya mawasiliano kwa Kiswahili kwa wanafunzi wa taaluma zote. Aidha, inapendekeza hatua madhubuti za kuendeleza Kiswahili zichukuliwe kwa nia ya kukitumia kama ngao ya kuwakinga Wakenya dhidi ya athari potoshi za utandawazi huku kikitumika kustawisha taasisi, kuunda mifumo na sera zenye manufaa ya kufaidi umma kipindi hiki cha utandawazi.

**Marejeleo**

- Mazrui, A. (1982). *Kilio cha Haki*. Nairobi: Longman.
- Atchson, J. (1991). *Language Change: Progress or Decay*. New York: Cambridge University Press.
- Chimerah, R. (1998). *Kiswahili, Past Present and Future Horizons*. Nairobi: Nairobi University Press.
- Chomsky, N. (1977). *Reflections on Language*. London: Fontana.
- IMF: In *The World Book Dictionary. Vol 23*. Chicago: World Book Inc.
- Makoti, V. S. (2008). Kiswahili: Matumizi na Uchumi. Katika: Nathan O. Ogechi, Naomi L. Shitemi na Kenneth I. Simala (Wah.) *Nadbaria katika Taaluma ya Kiswahili na Lugha za Kiafrika* (pp. 243 – 248). Eldoret: Moi University Press.
- Marshad, A. (1993). *Language Contact*. London: Edward Arnold.
- Massamba, D. P. B. (1986). On the Influence of Local Languages on Kiswahili: The case of Mara Region in Tanzania. In: *Kiswahili: Vol. 53/1* (67 – 83).
- Mkangi, K. G. C. (1984). *Mafuta*. Nairobi: Heinemann Education Books.
- Mohamed, S. A. (1995). *Dunia Mti Mkavu*. Nairobi: Longman.
- Msanjila, Y. P. (2005). Problems of Writing in Kiswahili: A Case Study of Kigurunyembe and Morogoro Secondary Schools in Tanzania. *Nordic Journal of African Studies. Vol. 14(1)* (15-25).
- Mukuthuria, M. (2006). Kiswahili and its Expanding Roles of Development in East African Cooperation: A Case of Uganda. In *Nordic Journal of African Studies* 15(2): (154-165).
- Mukuthuria, M. (2007). Mchango wa Tafsiri Katika Tanzu za Kitaaluma za Kiswahili katika Kimani Njogu (Mh.) *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya* (uk. 119-134). Nairobi: Taweza Communications.
- Mukuthuria, M. (2009). Islam and Development of Kiswahili”. *The Journal of Pan African Studies. Vol. 2 No. 8*. 36 - 45
- Njogu, K. (2007) (Mh). *Kiswahili na Elimu Nchini Kenya*. Nairobi: Twaweza Communications.
- Njogu, K. (2008). Kiswahili: The Language of Regional and National Integration. In. *Getting Heard: Reclaiming Performance Space in Kenya* (122 -147). Nairobi: Twaweza Communications.
- Oxford English Dictionary (1989). Oxford: Oxford University Press.
- Senkoro, F. K. (1982). *Fasihi*. Dar es Salam: Press and Publicity Centre.

- Thiong'o, N. (1986). *Decolonising the Mind: The Politics of Language in African Literature*. Portsmouth: J. Currey N.H; London: Heinemann.
- TUKI (1990). *Kamusi Sanifu ya Isimu na Lugha*. Dar es Salam: TUKI.
- TUKI (2004). *Kamusi ya Kiswahili Sanifu*. Dar es Salam: TUKI.
- Wa Mberia, K. (2001). *Kifo Kisimani*. Nairobi: Marimba Publications.
- Workbook Dictionary (1988). New York: Longman Publishers.
- Yuen, R. C. (1988). *The World Book Dictionary Vol. 23*. Chicago: World Book Inc.